



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO



Unapojibu tafadhali taja:

KUMB.NA. AC.216/275/01

TAREHE 12.09.2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA ZA VIBARUA KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo anapenda kuwatangazia nafasi za ajira za Mkataba wa Miezi Mitatu kwa Watanzania wenye sifa kama ifuatavyo:-

1.0 MKUSANYA USHURU (MAKARANI) - NAFASI 118

SIFA:

- Awe raia wa Tanzania
- Awe amehitimu na kupata Cheti cha Kidato cha Nne/Sita
- Asiwe mwajiriwa wa Serikali
- Awe na umri kati ya miaka 18 – 45
- Muadilifu asiye na kasoro yoyote
- Awe na uwezo wa kutumia simu janja (Smartphone)

KAZI NA MAJUKUMU

- Kukusanya ushuru katika Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli
- Kukusanya ushuru katika masoko ya Manispaa
- Kutunza kumbukumbu za hesabu
- Kutunza vizuri mashine za kukusanyia mapato (POS)
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Msimamizi wake
- Kuwasilisha makusanyo katika Akaunti za Halmashauri
- Kutoa na kuwasilisha taarifa za makusanyo ya kila siku kwa Halmashauri.

MASHAHARA SHILINGI 200,000/= (LAKI MBILI KWA MWEZI)

NB: Waombaji wenye sifa zaidi ya zilizotajwa hapo juu maombi yao hayatafikiriwa

JINSI YA KUTUMA MAOMBI:

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono, zikiwa na anwani kamili ya Mwombaji pamoja na namba ya Simu na zitumwe kwa anuani ifuatayo:-

MKURUGENZI WA HALMASHAURI


MANISPAA YA UBUNGO

S.L.P. 55068

DAR ES SALAAM

TAREHE YA MWISHO YA KUPOKEA MAOMBI:

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **26/09/2022** saa 9.30 Alasiri.


Beatrice R. Dominic

MKURUGENZI WA MANISPAA

MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO
DAR-ES-SALAAM

Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa, Luguruni, Barabara ya Morogoro, S.L.P: 55068, Dar es Salaam,
Unaweza pia kuwasiliana nasi kwa Simu. 0222-926341, Nukushi: 0222-92342, Tovuti; www.ubungomc.go.tz,

Barua pepe; info@ubungomc.go.tz

